# 13 NJIA BORA ZAIDI YA KUUSHINDA MSONGO



Hivi leo tunaishi chini ya msongo, unyong'onyevu, na fadhaa, ambazo huathiri afya na furaha yetu. Asilimia 70 hadi 90 ya magonjwa yote ni ya kiakili, kama matokeo ya fadhaa zetu. Tunahitaji pumziko la kimwili na kiroho, ili kuyajua sana mambo ya nafsi yetu ya ndani pamoja na kufahamiana na Muumba wetu, ambaye wengi wetu tumempuuzia ama hata kumkataa. Tunapouchunguza uumbaji, tunashangaa. Chukulia kwa mfano, kuzaliwa kwa mtoto, kiumbe awezaye kuona, kusikia, kujisogeza, na kutoa sauti. Akili za mwanadamu, pamoja na uwezo wake mwingi wa kutafakari; jicho lilivyo na utendaji wake wa kustaajabisha; na pale tunapoziangalia nyota katika anga la juu, ama unapowaangalia viumbe walio wadogo sana, uyaangalie yale maua mazuri ya kupendeza bustanini, mwangalie mchanga akitabasamu, hatuna jingine isipokuwa kumtukuza Mungu. Zaburi 139:13, 14.

## *HEBU NA TUMTUKUZE MUUMBA!*

**1. Je, Mungu anastahili nini kwa ajili ya yale aliyoyaumba? Ufunuo 4:11.**

______________________________________________________________

**2. Je, Mungu alihitaji maelefu ya miaka ili kuiumba dunia? Ilimchukua muda gani? Mwanzo 1:31.**

______________________________________________________________

- *Katika siku ya kwanza, Mungu aliumba nuru (Mwanzo 1:1-5). Dunia ilikuwa tupu na ukiwa.*
- *Katika siku ya pili, aliumba anga na mbingu (mstari wa 6-8).*
- *Katika siku ya tatu, aliumba nchi na mimea (mstari wa 9-13).*
- *Katika siku ya nne, alipangilia mfumo wa anga (jua, mwezi, na nyota (mstari wa 14-19).*
- *Katika siku ya tano, aliumba samaki na ndege (mstari wa 20-23).*
- *Katika siku ya sita, aliumba wanyama wa nchi pamoja na mwanadamu (mstari wa 24-28, 31).*

**3. Je, alifanya nini panapo siku ya saba? Mwanzo 2:1-3.**

*Mungu* ________________________________________ *siku ya saba.*

a) Mungu hakupumzika kwa sababu amechoka bali kutupatia sisi kielelezo.

b) Mungu hakibatilishi kile alichokibariki na kukitakasa. Hesabu 23:19, 20.

*Minara (sanamu) ya kumbukumbu imejengwa mara nyingi ili kuwaheshimu watu wakubwa, kama vile wapigania uhuru, mashujaa, washairi, wavumbuzi, walimu, kina mama, watu walioitumikia jamii ama kuokoa maisha. Kule Bern, Uswisi kuna kumbukumbu ya mtakatifu Bernard aliyewaokoa watu 14 katika milima ya Alps.*

**4. Je, ni kumbukumbu gani iliyowekwa katika amri ya nne ya Sheria Takatifu ya Mungu ili kumheshimu Yeye kama Muumba? Kutoka 20:8-11.** ______________________________

## *KUITUNZA SIKU YOTE YA SABATO*

**5. Je, Mungu anaionje Sabato? Ezekieli 20:12, 20.** ______________________________

*Muhuri ina vipingee vitatu: 1. Jina, 2. Cheo, 3. Eneo la mamlaka. Katika ile amri ya nne (Kutoka 20:8-11) tunavikuta vipengee hivi ifuatavyo:*

**1. Jina:** Bwana Mungu wako. **2. Cheo:** Muumba (Mungu aliumba…..). **3. Eneo la mamlaka:** Mbingu na nchi.

**6. Je, Sabato ilipata kuadhimishwa kabla ya kutolewa kwa ile sheria katika Mlima Sinai? Kutoka 16:15, 21 -30.** __________________________________________

*Uthibitisho wa jambo hili ni muujiza wa ______________________. Tangia pale, utaratibu wa juma haujapata kubadilishwa katika kalenda ya Wayahudi wa kale, wala katika kalenda yetu sisi wenyewe.*

**7. Je, Isaya ameielezeaje siku ya Sabato? Isaya 58:13, 14. ___________________________**

**8. Je, hii Sabato iliwahusu waumini wasio Wayahudi wa Agano la Kale na Wakristo wa leo pia? Isaya 56:2-7. _______________________________________________________________**

## *JE, YESU NA WANAFUNZI WAKE WALITUNZA SABATO?*

**9. Uhusiano wa Yesu na Sabato ukoje?**

*a) Kristo Mwenyewe ndiye aliyeiumba. Yohana 1:1-14; Wakolosai 1:15-17.*
*b) Aliitangaza ile sheria katika Mlima Sinai. Nehemia 9:12, 13; 1 Wakorintho 10:4.*

**10. Je, desturi ya Yesu ilikuwaje pale alipokuwapo hapa duniani? Luka 4:16, 31.**

_______________________________________________________________

**11. Je, Sabato ilifanywa kwa ajili ya watu wote? Marko 2:27, 28. ____________________**

*a) Yeye ndiye Bwana, Mmiliki na Mwanzilishi wa Sabato, kwa hiyo ni siku ya Bwana.*
*b) Alifundisha jinsi ya kuitunza kwa kutenda mema na kuhubiri panapo siku hii. Mathayo 12:27, 28.*

**12. Je, Mariamu mama yake Yesu pamoja na wanawake wengine waaminifu waliofundishwa na Yesu, walifanya nini baada ya kusulubiwa Kwake? Luka 23:56.**

_______________________________________________________________

**13. Je, Sabato ingeendelea kuwa takatifu hata baada kifo cha Kristo? Ni ushauri gani aliowapatia wanafunzi Wake pale alipowaelezea juu ya kuangamizwa kwa Yerusalemu, jambo ambalo lilitokea zaidi ya miaka 40 baadaye (mwaka 70 B.K.)? Mathayo 24:20.**

_______________________________________________________________

**14. Je, mitume nao walitunza Sabato?**

a) Kule Korintho. Matendo 18:3, 4.
b) Kule Thesalonike. Matendo 17:2, 3.
c) Kule Antiokia. Matendo 13:14, 42, 44.
d) Kule Filipi, kando ya mto. Matendo 16:13.

**15. Je, ni wapi ambako Sabato itatunzwa milele? Isaya 6:22, 23. ______________________**

- Yesu alieleza ya kwamba Sabato ilifanywa kwa ajili ya kumfaidia mwanadamu. Marko 2:27.
- Ni njia bora zaidi ya kuushinda msongo pamoja na unyong'onyevu. Inatupatia pumziko la mwili, nafsi na roho.
- Ni siku ya kuwasiliana na Yesu pale tunapokutanika pamoja, kama vile alivyofanya Yeye. Hivyo, tunaimarisha uhusiano wetu pamoja Naye, nasi tunafunguka kutoka katika msongo wa kisaiklojia na kupata pumziko na amani ya nafsi yetu. Mathayo 11:28-30.
- Tunamheshimu Muumba wa uhai pale tunapofurahia mambo ya asili na kumpatia heshima, utukufu na uweza wa kuumba kila kitu.
- Ni siku ya kuiweka wakfu familia na kuwafundisha watoto wetu juu ya njia za Mungu.

**16. Je, yawezekanaje kuitunza siku hii takatifu katika dunia iliyopinduka juu chini? Wafilipi 4:13; Zaburi 37:3-5; Isaya 65:13. ____________________________________________**

*Tunapata furaha pale tunapoonyesha upendo wetu kwa Mungu! Tutapata dhamira iliyotakata pamoja na uhakika wa kukamilika kwa wajibu wetu.*

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba Sabato ni siku sahihi ya kupumzika nami ninapenda kuitunza.*

○ *Ndio* ○ *Hapana*

---